OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

HALMASHAURI YA MANISPAA TEMEKE

Kibasila Shule ya Sekondari,

S.L.P. 20378,

DAR ES SALAAM.

Jina la Mwanafunzi……..

Fomu……..

YAH; MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIBASILA WILAYA YA TEMEKE MKOA WA DAR ES SALAAM. MWAKA……..

- Ninafuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka 2021 katika Shule ya Sekondari Kibasila. HONGERA SANA. Shule hii ipo katika kata ya Miburani Wilaya ya Temeke inatazamana na kiwanda cha Serengeti karibu na makutano ya barabara ya Mandela na Chang'ombe.

  Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ……. Unatakiwa kiripoti shule tarehe ……

- Mambo muhimu ya kuzingatia;
  - **Sare za shule;**
    - **Sare za shule kwa wasichana;**
      - Sketi mbili (2) za kijani nzito kitambaa cha takroni ndefu zinazovuka magoti.
      - Sweta rangi ya kijani linalofanana na sketi ya shule
      - Shati mbili (2) nyeupe tetroni mikono mifupi

- Nguo itakayovaliwa ndani ya shati iwe nyeupe vesti au singlet
- Maelezo ya vipimo na aina ya mshono wa sketi utaelekezwa shuleni.

- Viatu vya ngozi nyeusi (jozi mbili) viwe vya kufunga na kamba na visiwe na kisigino kirefu na visiwe vinavyopiga kelele. Viwe vinafunika kabisa (visiwe vya wazi), wala kuchongoka.
- Soksi nyeupe ndefu (stocking) sio za kuonyesha mwili (lesi)
- **Begi Jeusi** la kubebea vitabu lisilofanana na kikapu na lisiwe la kitambaa cha nguo.

- **Sare za Wavulana;**
  - Suruali mbili (2) kitambaa cha takroni rangi ya khaki, zisiwe za kubana mwili.
  - Mkanda mweusi wa Ngozi.
  - Shati mbili (2) tetroni mikono mifupi.
  - Nguo ya kuvalia ndani iwe nyeupe vesti au singlet.
  - Viatu vya ngozi vyeusi jozi (2) vya kufunga na kamba, visiwe vya wazi wala kuchongoka.
  - Sweta rangi ya kijani tupu.
  - Sampuli ya kitambaa cha suruali imeambatanishwa na fomu.
  - Maelekezo ya vipimo na aina ya mshono wa suruali /utaelekezwa shuleni wakati wa kuchukua fomu.

- **VIFAA BINAFSI VYA MWANAFUNZI.**
  - Mkebe wa vifaa vya Hisabati. (mathematical set instruments)
  - Peni, rula na Penseli.
  - Madaftari makubwa (counter book) 12
  - Dictionary/kamusi ya kiingereza
  - Mathematical Table (log table)

- Vitabu (orodha ya vitabu vinavyotakiwa watapewa na walimu wao wa masomo).
- Passportsize **04** zenye background ya blue.

- **SHERIA NA KANUNI ZA MUHIMU ZA SHULE HII.**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978.

Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

- Heshima kwa walimu, viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- Lugha chafu/matusi haziruhusiwi shuleni.
- Maudhurio mazuri katika shughuli ndani na je ya shule ni muhimu.
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- Kuvaa nguo za shule wakati wote unapotakiwa
  - Sketi ya shule ivaliwe kiunoni(isiwe mlegezo) na iwe ndefu chini ya magoti
  - Suruali ya shule iwe na malinda mawili mbele upana wa suruali chini usipungue inchi 16-18 yenye turn up.
  - Mashati meupe yasiwe ya kubana wala yasiwe mafupi ya valiwe kwa kuchomekea nay awe na nembo ya shule.
  - Sare za shule zitakazo kiuka utaratibu hapo juu zitachanwa.
  - Siku zisizokuwa za masomo iwapo mwanafunzi atatakiwa kufika shuleni kwa sababu yeyote ile atatakiwa afike akiwa amevaa sare za shule.
- Kuzingatia ratiba za shule wakati wote.
- Nywele fupi, zisizo na mitindo wala kuwekwa dawa, zenye urefu usiozidi unene wa njiti ya kiberiti na si kipara.
- Ni marufuku kufuga ndevu
- Huruhusiwi kufuga kucha, kupaka rangi, kuvaa bangili,herein na mikufu ndani ya sare ya shule.

- Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutumia muda wa masomo vizuri ni marufuku kupiga kelele uwapo darasani/wakati wa masomo.
- Ni marufuku kuwepo ndani ya eneo la shule baada ya saa 11;30 jioni (kama hakuna shughuli maalum ya kishule)

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE

- Wizi.
- Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro.
- Kugoma na kuhamasisha mgomo.
- Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujuma.
- Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, Kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
- Kusuka nywele kwa mitindo isiyokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi unaokubalika na uongozi wa shule.
- Kufuga ndevu.
- Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
- Uvutaji wa sigara.
- Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
- Kupata ujauzito au kutoa ujauzito.
- Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
- Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
- Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
- Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
- Kudharau bendera ya Taifa.
- Kufanya jaribio la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
- Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.
- Kunyoa vipara, kunyoa nyusi
- Hauruhusiwi kuvaa mabuti au viatu vinavyofanana na jeshi
- Mashati makubwa sana slim fiti hayaruhusiwi

- Kuvaa pete herein
- Kufuga kucha(ndefu)
- Kupaka hina rangi ya kucha piko, wanja
- Kukali au kulilax ni marufuku
- Kunyoa mitindo
- Kuvaa mikanda isiyoendana na vazi rasmi la shule.

3.2 SHERIA YA JUMLA

Kila wakati fikiria kwanza kabla ya kunena na tumia busara kutenda

3.3. ADHABU

- Adhabu zitaweza kutolewa na mwalimu yeyote kwa mwanafunzi anaye onesha utovu wa nidhamu.

- Kiranja pia anaruhusiwa kutoa adhabu kulingana na kosa lililotendwa na mwanafunzi ilimradi asipige kiboko au kuzuia kuingia darasani wakati wa masomo.

- Kosa linapokuwa kubwa litaandikwa katika jalada la mwanafunzi na kitabu cha kumbukumbu za adhabu.

3.4 MAMBO MENGINE MUHIMU

Wanafunzi wote wanatakiwa kutunza kwa uwezo wao wote mali na vyombo vya shule vilivyo chini ya uangalizi wao.

- Hakuna chombo au kifaa ha aina yoote kinachoruhusiwa kutoka mahali pake kwa matumizi au shughuli zisizo idhinishwa
- Iwapo chombo kimehamishwa kwa shughuli maalum ni lazimna kirudishwe mahali pake mara tu baada ya matumizi husika.
- Uhalibifu au upotevu wa kifaa chochote cha shule kwa makusudi ama uzembe lazima ufidiwe na muhusika.
- Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa Hospital ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara ufikapo shuleni.

- Usiandike mahali pasipo husika kama vile kutani, vitabuni kwenye samani za shule n.k
- Usimpige au kumshambulia mwanafunzi mwenzako ama ata mtu mwingine yeyote
- Usikatae uteuzi kushiriki shughuli mbalimbali kama vile michezo, maandamano uwakilishi n.k
- Usigune wala kuzomea wakati mwalimu au kiongozi yeyote anapotoa matangazo.
- Usibandike tangazo lolote bila ruhusa ya mwalimu anayehusika na mada ya tangazo hilo.
- Hotuba zote lazima zionwe na mkuu wa shule, kabla ya kutolewa katika hadhara yoyote shuleni.
- Usifanye mkutano bila ya ruhusa ya mwaliu anaye husika kukilea kikundi kinachohusika.
- Usihubiri dini,siasa au jambo lolote sala zote zianyike mahali panapohusika kama vile kanisani au msikitini.

FOMU YA USAJILI (IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI)

A: IJAZWE NA MWANAFUNZI:

- Jina kamili la mwanafunzi……....
- PICHA
- MWANAFUNZI
- Taifa……
- Uraia…….. Picha ya mwanafunzi
- Dini……..
- Tarehe ya kuzaliwa……
- Mahali alipozaliwa…… Wilaya……
- Shule aliyosoma kabla ya kuja shule ya sekondari

  ……

Shule ya msingi	Tarehe na mwaka aliomaliza	Tarehe na mwaka aliotoka
I		
II		
III		
IV		

8. Nakala ya cheti cha kuzaliwa

9. Saini ya mwanafunzi ……..

B: MAELEZO BINAFSI YA MZAZI /MLEZI:

- PICHA
- MZAZI

- Jina kamili……..
- Utaifa …… ……
- Uraia……
- Anuani kamili mjini Dar es salaam……
- Sehemu unayoishi……... Picha ya Mzazi/Mlezi
- Mtaa……..
- Namba ya nyumba…….
- Simu ya mkononi: Baba/mlezi…….. Mama/ Mlezi……

C: MAELEZO YA KIKAZI YA MZAZI/ MLEZI:

- Jina la mwajiri na Idara…….
- Kazi ya mzazi/ Mlezi (Meneja, Daktari, Mfanyabiashara n.k)……..

D: SOMO LA DINI

Mimi……ambaye ni Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.....Kidato cha…… Ninaruhusu mtoto wangu kuhudhuria somo la dini ya …… Dhehebu la ……. Siku ya IJUMAA akiwa shuleni Kibasila sekondari.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi……